**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MUSOMA**
**ILIYOKETI MUSOMA**

**SHAURI LA MAREJEO YA GHARAMA NA. 3418/2024 LA MWAKA 2024**

**MAGESA MAGORI..........................................................MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**JEREMIA RUKONDO (Msimamizi wa Mirathi**
**ya Marehemu Dishon Rukondo) .......................................MJIBU MAOMBI**

**UAMUZI WA RIDHAA**

28/05/2024 & 30/05/2024

**Kafanabo, J**.:

Uamuzi huu wa ridhaa unatokana na maombi ya marejeo ya gharama yaliyowasilishwa katika mahakama hii mnamo tarehe 21/02/2024 yakihusisha wadaawa waliotajwa. Maombi haya ya marejeo yanatokana na uamuzi wa tarehe 04/12/2023 katika Shauri la Gharama Namba 942 la Mwaka 2021 uliotolewa na Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Musoma, Mkoa wa Mara.

Katika Mahakama hii, Mleta Maombi aliwasilisha maombi ya marejeo ya uamuzi uliotajwa dhidi ya Mjibu Maombi akiomba nafuu zifuatazo:

1. *Mahakama ichunguze, ibadilishe na kutengua Amri ya Mahakama (ya Afisa Mtozaji) ya tarehe 04/12/2023 ya Shauri la Gharama Namba 941 la Mwaka 2023 na kuelekeza kwamba shauri hilo la gharama lisikilizwe na kutolewa uamuzi kwa mujibu wa sheria mbele ya Afisa Mtozaji Mwingine.*
2. *Amri yeyote Ambayo Mahakama itaona yafaa kwa mujibu wa hali ya Shauri.*

Hata hivyo, kabla ya maombi hayo ya marejeo kusikilizwa, mnamo Tarehe 28/05/2024 wadaawa wote wawili pamoja na Mawakili wao, Bw. Daudi Mahemba, Wakili Msomi akimuwakilisha Mleta Maombi na Bw.

Ostack Mligo, Wakili Msomi akimuwakilisha Mjibu maombi, walifika mbele ya Mahakama hii na kuifahamisha Mahakama kuwa wamefikia Muafaka na makubaliano ya kumaliza tofauti zao na mgogoro uliopo Mahakamani kwa hiyari na ridhaa yao wenyewe kwa mujibu wa Hati ya Maridhiano iliyosainiwa tarehe 27/05/2024 na kuwasilishwa kwenye Mfumo wa kielektroniki wa Mahakama mnamo Tarehe 28/05/2024.

Hivyo, wadaawa waliotajwa kupitia kwa mawakili wao, huku wadaawa wenyewe wakiwa wamehudhuria Mahakamani, kwa kauli moja, waliiomba Mahakama iamuru kuwa shauri hili limepata suluhu ya hiyari ya wadaawa kwa mujibu wa hati ya maridhiano.

Kwamba baada ya Mahakama hii kupitia hati ya maridhiano na kujiridhisha kuwa imetimiza vigezo vya kuwa hati inayoweza kusajiliwa kama uamuzi wa mahakama, na kwa kuzingatia **Amri ya XXIII, Kanuni ya 3 ya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai (Sura ya 33, Kama Ilivyorejewa Mwaka 2019,** Mahakama hii inaamuru kwamba shauri hili limepata suluhu kwa amri zifuatazo:

a) Kwamba Magesa Magori na Jeremia Rukondo, ambao ni majirani huko Bweri Senta, Manispaa ya Musoma, Mkoa wa Mara, ambao maeneo yao ya mgogoro yanapakana, wameridhia kuwa katika upande wa nyuma (uani) wa nyumba ya Bw. Magesa Magori inayopakana na eneo la makazi la Bw. Jeremia Rukondo, Bw. Magesa Magori ataongeza ukuta wa uzio wa matofali kuanzia kwenye kona ya mashariki mwa nyumba yake hadi kwenye kona ya kaskazini mwa karo la choo/maliwato yake. Pia kutoka hapo kwenye kona ya kaskazini mwa karo la choo/majitaka, ukuta wa matofali utajengwa kuelekea magharibi mwa karo hilo kwa mita nne; kisha ukuta wa matofali utajengwa kuelekea upande wa kusini na kuunganishwa na ukuta wa choo/maliwato ya Magesa Magori.

b) Kwamba Bw. Magesa Magori na Bw. Jeremia Rukondo pia wameridhia kuwa katika upande wa mbele kuelekea barabara kuu itokayo Musoma kwenda Makutano (zero zero), uchochoro unaotenganisha nyumba zao umegawanywa nusu kwa nusu, ambapo kigingi cha matofali kitachimbiwa katikati ya uchochoro huo kama alama ya mpaka. Magesa Magori atamiliki nusu ya uchochoro huo na Jeremia Rukondo atamiliki nusu nyingine ya uchochoro huo unaotenganisha nyumba zao. Wadaawa hawa

wameridhia kuwa kila mmoja asijenge aina yoyote ya jengo katika nusu yake ya uchochoro, ama jengo kubwa au dogo, ama la kudumu au la muda mfupi; bali kila mmoja wao anaweza kuitumia nusu yake ya uchochoro kwa shughuli mbali mbali za kibinadamu kama vile kuhifadhi vifaa vya kazi kwa muda, kustarehe kwa kula na kunywa, kufanya vikao, na kulifanyia usafi, lakini wasijenge majengo ya aina yeyote, isipokuwa wanaweza kusimika hema na kisha kuliondoa baada ya shughuli iliyokusudiwa kumalizika.

c) Kwamba, Magesa Magori ameridhia kuondoa na ataondoa msingi wa mawe aliokwisha kuujenga kwenye nusu yake ya eneo la uchochoro, aliweke eneo hilo safi na wazi.

d) Kwamba, mipaka ya misingi ya nyumba za wadaawa ibaki kama ilivyo sasa, isisogezwe hata kidogo kwa kisingizio cha kufanya ukarabati wa msingi; isipokuwa endapo msingi wa nyumba ya mdaawa mmojawapo utahitaji ukarabati kutokana na uchakavu, basi ukarabati huo utafanywa bila kusogeza mpaka wa msingi wenyewe.

e) Kwamba, Magesa Magori na Jeremia Rukondo wameridhia kuondoa mashauri yao yaliyokuwa yakiendelea mahakamani; badala yake wamekubali kuzingatia maridhiano haya ambayo wamekiri kwamba ni bora zaidi ya hukumu zote za mahakama mbali mbali walikopitia kwa muda wa miaka mingi ya undeshaji wa kesi baina yao kuhusu mgogoro huu.

f) Kwamba, familia ya Magesa Magori na familia ya Jeremia Rukondo zimehudhuria mazungumzo ya maridhiano na wote kwa pamoja wameyaafiki maridhiano haya.

g) Kwamba, baada ya maridhiano haya kusainiwa, mahakama itayafanya kuwa hukumu kati ya Mleta Maombi na Mjibu Maombi.

h) Kwamba, atayekiuka maridhiano haya hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Imeamuliwa hivyo na Mahakama.

Imesainiwa na kuwekwa muhuri wa Mahakama leo tarehe 30/05/2024

**K.I.Kafanabo**
**Jaji**

Uamuzi huu umesomwa leo tarehe 30/05/2024 mbele Bw. Daudi Mahemba, Wakili wa Mleta Maombi, huku akishika mikoba ya Bw. Ostack Mligo, Wakili wa Mjibu Maombi. Pia wadaawa wote wawili Bw. Magesa Magori na Bw. Jeremia Rukondo wamehudhuria.

**K.I.Kafanabo**
**Jaji**
**30/05/2024**